International
Labour
Office

# Pendekezo kuhusu VVU na UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi, 2010 (Na. 200)



ILO AIDS
www.ilo.org/aids

Hakimiliki © Shirika la Kazi Duniani 2010

Chapisho la Kwanza 2010

Machapisho ya Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani yanalindwa na hakimiliki chini ya kanuni ya 2 ya Mkataba wa Hakimiliki wa Kimataifa. Hata hivyo nukuu fupifupi zinaweza kutumiwa bila kuomba kibali ilimradi chanzo cha nukuu hizo kimeonyeshwa waziwazi. Lakini mtu yeyote anayetaka kurudufisha au kutafsiri machapisho ya ILO sharti aombe kibali kutoka kwa Taasisi ya Uchapishaji (Haki na Vibali), Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani, CH-1211 Geneva 22, Switzerland, au kwa barua pepe: pubdroit@ilo.org. Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani inakaribisha maombi kama hayo.

Maktaba, taasisi na watumiaji wengine wanaweza kunakili kwa mashine machapisho ya ILO kulingana na leseni walizopewa kwa ajili hiyo. Tembelea www.ifrro.org ili kuweze kuona haki za kurudufu nchini mwako.

*Pendekezo kuhusu VVU na UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi, 2010 (Na. 200)*
Shirika la Kazi Duniani -Geneva: ILO, 2010 12 p.

ISBN: 978-92-2-923819-7 (print); 978-2-92-2923820-3 (Web pdf)

HIV / AIDS / occupational health / occupational safety / workers rights / ILO Recommendation / text
15.04.2

Pia linapatikana kwa Kifaransa: *Recommandation concernant le VIH et le sida et le monde du travail, 2010 (n° 200)*

[ISBN 9789222238194 (print); 9789222238200 (Web pdf)], Geneva, 2010;
na kwa Kihispania: *Recommendación sobre el VIH y el sida y el mundo del trabajo, 2010 (núm. 200)* [ISBN
9789223238193 (chapisho); 9789223238209 (Web pdf)], Geneva, 2010.

*Katalogi ya ILO katika Data ya Machapisho*

Maelezo yaliyotumika katika machapisho ya ILO, ambayo yanazingatia taratibu za Umoja wa Mataifa pamoja na mfumo wa mpangilio uliotumika ndani ya machapisho hayo havitoi msimamo wowote wa Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au kanda yoyote au viongozi wake, au kuhusiana na mipaka ya maeneo hayo.

Wajibu kuhusiana na maoni yaliyotolewa katika makala zilizosainiwa, tafiti au michango mingine ya maandishi yanabebwa na waandishi wenyewe na wala Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani haichukui jukumu lolote kuhusiana na maoni yaliyotolewa ndani yake kutokana na kuwa mchapishaji wa maandishi hayo.

Marejeo ya majina ya makampuni na bidhaa za kibiashara pamoja na michakato mbalimbali haina maana kwamba Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani inakubaliana nayo wala kukosa kutaja kampuni mahususi, bidhaa ya kibiashara au mchakato fulani hakumaanishi kwamba ILO haitambui vitu hivyo.

Machapisho ya ILO yanaweza kupatikana kupitia maduka makubwa ya kuuza vitabu au kutoka ofisi za ILO katika nchi yoyote ile, au moja kwa moja kutoka "ILO Publications, International Labour Office, CH-1211 Geneva 22, Switzerland". Aidha katalogi au orodha za machapisho mapya zinapatikana na kutolewa bure kupitia anwani hiyo iliyotolewa, au kwa barua pepe: pubvente@ilo.org

Tembelea tovuti yetu: www.ilo.org/publns

Kimechapishwa Dar es Salaam, Tanzania

**Dibaji**

Kijitabu hiki kina maelezo ya Pendekezo la Shirika la Kazi Duniani (ILO) kuhusu **VVU na UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi**, 2010 (Na. 200), na Uamuzi kuhusu namna ya kuhamasisha na kutekeleza Pendekezo hili ambalo linaonekana kuungwa mkono na pande zote tatu za Shirika la Kazi Duniani (serikali, vyama vya wafanya kazi na vile vya waajiri)

Kuenea kwa VVU ni moja ya changamoto kubwa zaidi katika sekta za afya, maendeleo, uchumi na maendeleo ya jamii inayoukabili ulimwengu leo hii. Katika nchi ambazo zimeathirika zaidi, athari ya VVU na UKIMWI umemomonyoa faida ya maendeleo ya miongo kadhaa, umevuruga uchumi na kuyumbisha jamii mbalimbali. VVU vinatarajiwa kuendelea kuongoza kwa kusababisha vifo na magonjwa katika nchi nyingi na watu wengi.

VVU umeweka kikwazo kikubwa katika kufanikisha kazi zenye staha na maendeleo endelevu. Umesababisha kupoteza maisha ya mamilioni ya watu wanaoishi na VVU na UKIMWI. Athari zake ni nyingi miongoni mwa vikundi vya watu wengi walio na umri wa kufanya kazi na husababisha gharama kubwa kwa makampuni kwa kusababisha kushuka kwa uzalishaji, ongezeko la gharama za uzalishaji na kupoteza watu wenye ujuzi na uzoefu. Kwa kuongezea, haki za msingi mahali pa kazi mara nyingi huvunjwa kutokana na kuwa na au kuhisiwa kuwa na VVU, hususan kutokana na ubaguzi na unyanyapaa wanaofanyiwa wafanyakazi wanaoishi au walioathirika na VVU na UKIMWI. Mbaya zaidi, ni kuwa hali ya kuenea kwa ugonjwa huu inaelekea kuandama jamii iliyokwishaathirika, hususan huathiri makundi ya watu ambao tayari wapo katika mazingira magumu au wamewekwa pembezoni.

Ulimwengu wa kazi unachukua nafasi muhimu katika kupambana na VVU na UKIMWI. Unatoa nafasi muhimu ya kuwafikia wanawake na wanaume wafanyakazi mahali ambapo wanatumia muda mwingi wa maisha yao: mahali pa kazi. Utungaji na utekelezaji wa sera na programu za mahali pa kazi kuhusu VVU na UKIMWI huwezesha kupatikana kwa huduma za kinga, matibabu, matunzo na msaada kwa ajili ya wafanyakazi na familia zao na wategemezi, hatimaye pia kuifikia jamii pana. Lakini hata hivyo, nafasi muhimu ya ulimwengu wa kazi katika kupambana na kuenea kwa ugonjwa huu bado haijatumiwa kikamilifu. Ili kutoa mchango kamili katika kushughulikia tatizo la kuenea kwa ugonjwa huu, ni muhimu hatua zitakazochukuliwa katika ulimwengu wa kazi ziwe sehemu ya sera, programu na mikakati ya taifa ya VVU na UKIMWI.

Mnamo mwaka 2001, ILO ilipitisha Kanuni za Utendaji kuhusu VVU/UKIMWI na ulimwengu wa kazi, ambazo zilikubaliwa na wengi na kutumika katika nchi nyingi. Mnamo mwaka 2007, pande zote tatu za Shirika la Kazi Duniani ziliamua kuwa wakati umefika wa kuanzisha mapambano ya ulimwengu wa kazi dhidi ya VVU na UKIMWI katika ngazi mbalimbali kwa kutunga na kupitisha viwango vya kazi vya kimataifa. Pendekezo Na. 200 limetokana na msimamo wa pamoja uliowekwa na pande tatu za ILO za Mataifa wanachama na wawakilishi wa waajiri na wafanyakazi, kwa ushirikiano wa karibu na vyama vya watu wanaoishi na VVU na mashirika ya kimataifa yanayoshirikiana na ILO, hususan UNAIDS, kuchunguza kwa kina mchango ambao ulimwengu wa kazi unaweza kuutoa kwa kuhakikisha kupatikana kwa huduma za kinga, matibabu, matunzo na msaada kwa wote.

Pendekezo hili linaonyesha haja ya kuimarisha juhudi za kutoa kinga mahali pa kazi na kuwezesha upatikanaji wa matibabu kwa watu wanaoishi au walioathirika na VVU na UKIMWI. Linahimiza kubuni na kutekeleza sera na programu za taifa za utatu kuhusu VVU na UKIMWI kwa kuziingiza kwenye sera na mikakati ya taifa ya jumla kuhusu VVU na UKIMWI na katika maendeleo na hifadhi ya jamii. Linahimiza kuheshimu haki za msingi za binadamu kwa wafanyakazi wote, pamoja na kuheshimu kanuni ya usawa wa kijinsia na haki ya mtu kutolazimishwa kupima na kueleza hali yake ya VVU, wakati huo huo likiwa linahimiza kila mmoja kupata kwa siri ushauri na kupima VVU kwa hiari mapema iwezekanavyo. Pendekezo hili pia linaziomba Nchi wanachama kutekeleza masharti yake kwa kufanya marekebisho ya sheria za nchi na kuzipitisha inapowezekana.

Iwapo wafanyakazi watakuwa hawafanyiwi unyanyapaa na ubaguzi kutokana na hali yao halisi ya VVU au kwa kuhisiwa, wao na wategemezi wao watanufaika kutokana na kupata elimu ya VVU, habari, matibabu, matunzo na msaada katika ngazi za taifa na mahali pa kazi. Upatikanaji huo wa huduma huwasaidia kuendesha maisha marefu na yenye kipato na kuchangia katika uchumi wa taifa na jamii.

Kwa kuzingatia Pendekezo na Suluhisho lake, ILO imeweka msimamo wa kuimarisha hatua zake za kuunga mkono utekelezaji wa misimamo ya kimataifa na kitaifa ili kulinda haki na utu wa wafanyakazi na watu wote wanaoishi na au walioathirika na VVU na UKIMWI.

Geneva, Juni 2010

Juan Somavia,
Mkurugenzi Mkuu

**Pendekezo Namba 200**

## PENDEKEZO KUHUSU VVU NA UKIMWI NA ULIMWENGU WA KAZI

Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Shirika la Kazi Duniani,

Baada ya kuitishwa huko Geneva na Uongozi wa Shirika la Kazi Duniani, na baada ya kukutana kwenye Kikao chake cha 99 tarehe 2 Juni 2010, na

Kuelewa kuwa VVU na UKIMWI una athari kubwa kwa jamii na uchumi, kwa ulimwengu wa kazi katika sekta zote mbili, sekta rasmi na isiyo rasmi, kwa wafanyakazi, familia zao na wategemezi wao, kwa vyama vya waajiri na wafanyakazi na kwa kampuni za umma na binafsi, na kukwamisha juhudi za kufanikisha kazi zenye staha na maendeleo endelevu, na

Kusisitiza tena nafasi muhimu ya Shirika la Kazi Duniani katika kushughulikia VVU na UKIMWI katika ulimwengu wa kazi na haja ya Shirika hili kuimarisha juhudi zake za kufanikisha haki ya kijamii na kupambana na ubaguzi na unyanyapaa kutokana na VVU na UKIMWI katika vipengele vyote vya kazi na mamlaka yake, na

Kuhimiza umuhimu wa kupunguza uchumi usio rasmi kwa kufanikisha kazi zenye staha na maendeleo endelevu ili kuhamasisha vizuri zaidi ulimwengu wa kazi katika kushughulikia VVU na UKIMWI, na

Kukumbuka kuwa tofauti kubwa za kijamii na kiuchumi, kutopata taarifa na kukosa ufahamu, kutotunza siri na kukosa matibabu au kutofuata vya kutosha masharti ya matibabu, huongeza hatari ya maambukizi ya VVU, idadi ya vifo, idadi ya watoto ambao wamepoteza mzazi mmoja au wote wawili na idadi ya wafanyakazi wanaojishughulisha katika kazi zisizo rasmi, na

Kuzingatia kuwa umaskini, tofauti za kijamii na kiuchumi na ukosefu wa ajira huongeza hatari ya kukosa huduma za kinga, matibabu, matunzo na msaada, hivyo kuongeza hatari ya maambukizi, na

Kukumbuka kuwa unyanyapaa, ubaguzi na tishio la kupoteza ajira wanalopata watu walioathirika na VVU au UKIMWI ni vikwazo vinavyosababisha mtu kushindwa kujua hali yake ya VVU, hivyo kuongeza hatari kwa wafanyakazi kupata VVU na kuwanyima haki ya kijamii, na

Kukumbuka kuwa VVU na UKIMWI una athari mbaya zaidi kwa makundi ya watu walio katika mazingira magumu na hatari, na

Kukumbuka kuwa VVU huwaathiri wote wanaume na wanawake, ingawa wanawake na wasichana wapo katika hatari kubwa zaidi na hivyo kuwawezesha kupata kwa urahisi zaidi maambukizi ya VVU na wameathirika zaidi na kuenea kwa VVU ikilinganishwa na wanaume kutokana na tofauti za kijinsia, na hivyo kuwawezesha wanawake ni sababu muhimu katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, na

Kuhimiza umuhimu wa kuwalinda wafanyakazi kupitia programu pana za usalama na afya kazini, na

Kuhimiza umuhimu wa kanuni za utendaji za ILO *Kanuni za utendaji za ILO kuhusu VVU/UKIMWI na ulimwengu wa kazi*, 2001, na haja ya kuimarisha athari zake kwa kuzingatia kuwa kuna vikwazo na kasoro katika utekelezaji wake, na

Kukumbuka haja ya kukuza na kutekeleza Mikataba na Mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani na maazimio na mapendekezo mengine ya kimataifa ambayo yanahusiana na VVU na UKIMWI na ulimwengu wa kazi, pamoja na yale yanayotambua haki ya kupata huduma za afya za viwango vya hali ya juu na viwango vya maisha yenye staha, na

Kutambua nafasi maalum ya vyama vya waajiri na wafanyakazi katika kukuza na kuunga mkono juhudi za kimataifa katika kupambana na VVU na UKIMWI na kupitia ulimwengu wa kazi, na

Kutambua nafasi muhimu ya mahali pa kazi kulingana na taarifa kuhusu kinga, matibabu, huduma na msaada katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, na

Kuthibitisha haja ya kuendelea na kuongeza ushirikiano wa kimataifa, hususan katika muktadha wa Programu ya Pamoja ya Umoja wa Mataifa kuhusu VVU/UKIMWI, kwa kuunga mkono juhudi za kuyafanyia kazi Mapendekezo haya, na

Kutambua umuhimu wa ushirikiano katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa na vyombo vinavyoshughulika na VVU na UKIMWI, ikiwa ni pamoja na sekta ya afya na kushirikiana na vyama husika, hususan vile vinavyowawakilisha watu wanaoishi na VVU, na

Kuthibitisha haja ya kuweka viwango vya kimataifa ili kuziongoza serikali na vyama vya waajiri na wafanyakazi katika kufafanua nafasi na majukumu yao katika ngazi zote, na

Baada ya kuamua kupitisha mapendekezo fulani kuhusiana na VVU na UKIMWI na ulimwengu wa kazi, na

Baada ya kuamua kuwa mapendekezo haya yatachukua muundo wa Pendekezo;

Mkutano huu unapitisha leo tarehe kumi na saba ya mwezi Juni ya mwaka elfu mbili na kumi Pendekezo lifuatalo, ambalo linaweza kudondolewa kama Pendekezo la VVU na UKIMWI, 2010.

## I. FASILI

1. Kwa madhumuni ya Pendekezo hili:

(a) "VVU" linarejelea virusi vinavyosababisha upungufu wa kinga mwilini, virusi vinavyoharibu mfumo wa kinga ya binadamu. Maambukizi yanaweza kuzuiwa kwa kuchukua hatua sahihi;

(b) "UKIMWI" linarejelea upungufu wa kinga mwilini ambao ni matokeo ya ugonjwa kuwa katika hatua ya pili ya maambukizi ya VVU, na unaonekana kwa kuandamwa na magonjwa nyemelezi au saratani zinazohusiana na VVU, au yote mawili;

(c) "watu wanaoishi na VVU" ina maana watu walioambukizwa VVU;

(d) "unyanyapaa" lina maana dalili ya kijamii ambayo, ikihusishwa na mtu, kawaida husababisha kudharauliwa au husababisha kikwazo kinachomzuia mtu aliyeambukizwa au aliyeathirika na VVU kufurahia kikamilifu maisha ya kijamii;

(e) "ubaguzi" lina maana tofauti yoyote, kutengwa au upendeleo ambao unaleta athari ya kuondoa au kuvuruga fursa sawa au kutendea sawa katika ajira au kazi, kama ilivyorejelewa kwenye Mkataba wa Ubaguzi (Ajira na Kazi), 1958, na Pendekezo, 1958;

(f) "watu walioathirika" lina maana watu ambao maisha yao yamebadilishwa na VVU au UKIMWI kutokana na athari kubwa zaidi za maambukizi;

(g) "marekebisho yanayofaa" lina maana mabadiliko au marekebisho yoyote katika kazi au mahali pa kazi ambayo yanaweza kufanyika na kumwezesha mtu anayeishi na VVU au UKIMWI kuweza kupata, au kushiriki au kuendelea na ajira;
(h) "mazingira magumu" lina maana kutopata fursa sawa, kutengwa kijamii, ukosefu wa ajira, kutokana na sababu za kijamii, kitamaduni, kisiasa na kiuchumi ambazo zimemfanya mtu kuwa katika hatari ya maambukizi ya VVU na kuwa na UKIMWI;
(i) "mahali pa kazi" linarejelea mahali popote ambapo wafanyakazi wanafanya shughuli zao; na
(j) "wafanyakazi" linawarejelea watu wanaofanya kazi kwa kufuata utaratibu wa aina yoyote.

## II. MAWANDA

2. Pendekezo hili linawalenga:

(a) wafanyakazi wote wanaofanya kazi kwa kufuata mipango ya aina zote, na mahali pote pa kazi, pamoja na:
  (i). watu walio katika ajira au kazi yoyote;
  (ii). wale walio katika mafunzo, ikiwa ni pamoja na walio kwenye mafunzo kwa vitendo na wanafunzi wa fani za ufundi;
  (iii). wanaojitolea;
  (iv). watafuta kazi na wanaoomba kazi; na
  (v). wafanyakazi walioachishwa na waliosimamishwa;
(b) sekta zote za uchumi, ikiwa ni pamoja na sekta binafsi na ya umma na uchumi rasmi na usio rasmi; na
(c) majeshi ya ulinzi na huduma rasmi.

## III. KANUNI ZA JUMLA

3.Kanuni zifuatazo za jumla zitumike katika hatua zote zinazochukuliwa katika juhudi za kitaifa za kupambana na VVU na UKIMWI katika ulimwengu wa kazi:

(a) mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI yatambuliwe kuwa yanachangia katika kufanikisha haki za binadamu na uhuru wa msingi na usawa wa kijinsia kwa wote ikiwa ni pamoja na wafanyakazi, familia zao na wategemezi wao;
(b) VVU na UKIMWI utambuliwe na kuchukuliwa kama suala la mahali pa kazi, ambalo inabidi kujumuishwa miongoni mwa vipengele muhimu vya mapambano ya kitaifa, kikanda na kimataifa dhidi ya kuenea kwa ugonjwa kwa kuvishirikisha kikamilifu vyama vya waajiri na wafanyakazi;
(c) kusiwe na ubaguzi dhidi ya wafanyakazi au kuwanyanyapaa, hususan wale wanaotafuta kazi na wanaoomba kazi, kutokana na hali halisi au ya kuhisiwa kuwa na maambukizi ya VVU au kwa sababu kwamba wanatoka katika kanda za dunia au sehemu ya watu wanaochukuliwa kuwa katika hatari au kuwa katika mazingira hatarishi ya maambukizi ya VVU;
(d) kuzuia njia zote za maambukizi ya VVU iwe kipaumbele cha msingi;
(e) wafanyakazi, familia zao na wategemezi wao wapate huduma na manufaa ya kinga, matibabu, huduma na msaada kuhusiana na VVU na UKIMWI, na mahali pa kazi pachukue nafasi katika kuwezesha upatikanaji wa huduma hizi;
(f) ushiriki na kufanya kazi kwa wafanyakazi katika kuandaa, kutekeleza na kutathmini programu za kitaifa na za mahali pa kazi utambuliwe na kuimarishwa;

(g) wafanyakazi wanufaike kutokana na programu za kuzuia hatari maalum za maambukizi ya VVU kazini na magonjwa husika ya kuambukiza, kama vile kifua kikuu;

(h) wafanyakazi, familia zao na wategemezi wao wapate ulinzi wa mambo yao ya faragha ikiwa ni pamoja na siri kuhusiana na VVU na UKIMWI, hususan kuhusiana na hali zao za VVU;

(i) mfanyakazi yeyote asitakiwe kupima VVU au kufichua hali yake ya VVU;

(j) hatua za kupambana na VVU na UKIMWI katika ulimwengu wa kazi ziwe sehemu ya sera za maendeleo ya taifa, pamoja na zile zinazohusiana na kazi, elimu, hifadhi ya jamii na afya; na

(k) ulinzi wa wafanyakazi katika kazi ambazo zinawaweka kwenye hatari kubwa ya maambukizi ya VVU.

## IV. SERA NA PROGRAMU ZA TAIFA

4. Wanachama wanatakiwa:

(a) kupitisha sera na programu za taifa kuhusu VVU na UKIMWI na ulimwengu wa kazi na kuhusu usalama na afya kazini, pale ambapo hakuna; na

(b) kuingiza sera na programu zao kuhusu VVU na UKIMWI na ulimwengu wa kazi kwenye mipango yao ya maendeleo na mikakati ya kupunguza umaskini, pamoja na kazi zenye staha, biashara endelevu na mikakati ya kuzalisha kipato, iwezekanavyo.

5. Katika kuandaa sera na programu za kitaifa, mamlaka husika zizingatie kanuni za utendaji za Shirika la Kazi Duniani kuhusu VVU/UKIMWI za mwaka 2001, na marekebisho yoyote yaliyofanyika, kanuni nyingine husika za Shirika la Kazi Duniani, na miongozo mingine ya kimataifa iliyopitishwa kuhusiana na mada hii.

6. Sera na programu za kitaifa ziandaliwe na mamlaka husika, kwa kushauriana na vyama viwakilishi vya waajiri na wafanyakazi, na vilevile vyama vinavyowawakilisha watu wanaoishi na VVU, kwa kuzingatia mitazamo ya sekta husika, hususan sekta ya afya.

7. Katika kuandaa sera na programu za taifa, mamlaka husika zizingatie nafasi ya mahali pa kazi katika kuzuia, kutibu, kutoa huduma na msaada, ikiwa ni pamoja na kukuza masuala ya ushauri na upimaji kwa hiari, kwa kushirikiana na jamii ya wenyeji.

8. Wanachama wachukue kila fursa kusambaza habari kuhusu sera na programu zao kuhusu VVU na UKIMWI na ulimwengu wa kazi kupitia vyama vya waajiri na wafanyakazi, vyombo vingine husika vya VVU na UKIMWI, na njia za kusambaza habari kwa umma.

### *Ubaguzi na ukuzaji wa fursa sawa na kutenda haki*

9. Serikali, kwa kushauriana na vyama vya waajiri na nile vya wafanyakazi vyenye uwakilishi mkubwa zizingatie kutoa ulinzi sawa na ule unaopatikana chini ya Mkataba wa Ubaguzi (Ajira na Kazi), 1958, kuzuia ubaguzi kutokana na kujua hali halisi au kwa kumhisia mtu kuwa ana VVU.

10. Hali halisi au ya kuhisiwa kuwa na VVU isiwe msingi wa ubaguzi kwa kumzuia mtu kuajiriwa au kuendelea na ajira, au kumnyima fursa sawa kulingana na masharti ya Mkataba wa Ubaguzi (Ajira na Kazi), 1958.

11. Kuwa na au kutambulika kuwa na VVU isiwe sababu ya kuachisha mtu kazi. Kutokuwepo kazini kwa muda kutokana na ugonjwa au kufanya kazi za kuhudumia wagonjwa wenye magonjwa yanayohusiana na VVU au UKIMWI kuchukuliwe sawa kama inavyochukuliwa kutokuwepo kazini kutokana na sababu nyingine za kiafya, kwa kuzingatia Mkataba wa Kusitisha Ajira, 1982.

12. Iwapo hatua zilizopo za kupambana na ubaguzi mahali pa kazi hazitoshelezi kutoa ulinzi wa kutosha dhidi ya ubaguzi kuhusiana na VVU na UKIMWI, Wanachama wapitishe hatua hizi au wachukue hatua nyingine mpya zilizopo, na kuzitekeleza ipasavyo na kwa uwazi.

13. Watu wenye ugonjwa unaohusiana na VVU wasinyimwe fursa ya kuendelea kufanya kazi zao, kwa kufanya marekebisho ya kutosha ikibidi, kwa wakati wote wakiwa wazima kiafya kuweza kufanya hivyo. Hatua za kuwahamisha na kuwapanga upya watu hao ili waweze kufanya kazi kulingana na uwezo wao, kuwapatia kazi nyingine kwa kuwapatia mafunzo au kuwawezesha kurudi kazini ni jambo linalotakiwa kuhimizwa, kwa kuzingatia sheria za Shirika la Kazi Duniani na za Umoja wa Mataifa.

14. Hatua zichukuliwe ndani ya (au kupitia) mahali pa kazi kupunguza maambukizi ya VVU na kuondoa athari zake kwa:

(a) kuhakikisha haki za binadamu na uhuru wa msingi unaheshimiwa;
(b) kuhakikisha kuwepo usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake;
(c) kuhakikisha zinachukuliwa hatua za kuzuia na kupiga marufuku vurugu na unyanyasaji mahali pa kazi;
(d) kukuza ushiriki mkubwa wa wanawake na wanaume katika juhudi za kupambana na VVU na UKIMWI;
(e) kukuza ushiriki na uwezeshaji wa wafanyakazi wote bila kujali jinsia na kama wapo katika kundi la watu walio kwenye mazingira magumu au la; na
(f) kuhakikisha utunzaji wa siri za taarifa binafsi, ikiwa ni pamoja na taarifa za kiafya.

*Kuzuia maambukizi*

15. Mikakati ya kuzuia maambukizi irekebishwe kulingana na masharti ya kitaifa na aina ya mahali pa kazi, na izingatie matatizo ya kijinsia, kitamaduni, kijamii na kiuchumi.

16. Programu za kuzuia maambukizi zihakikishe:

(a) kuwa taarifa zinatolewa na kupatikana kwa usahihi, zinaenda na wakati, zinazofaa na zinatolewa kwa wakati kwa watu wote kwa muundo unaozingatia utamaduni na kwa lugha inayoeleweka kupitia njia mbalimbali zilizopo za mawasiliano;
(b) kunakuwa na programu pana ya elimu ya kuwasaidia wanawake na wanaume kuelewa na kupunguza hatari ya aina zote za maambukizi ya VVU, ikiwa ni pamoja na maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, na kuelewa umuhimu wa kubadili tabia hatarishi zinazosababisha maambukizi;

(c) hatua madhubuti za usalama na afya kazini zinachukuliwa ;
(d) hatua za kuwahimiza wafanyakazi kujua hali yao ya VVU kupitia ushauri na upimaji kwa hiari zinachukuliwa;
(e) upatikanaji wa njia zote za kinga, ikiwa ni pamoja na kuwahakikishia upatikanaji wa madawa na vifaa vya kutosha, hususan kondomu za kiume na kike na, ikiwezekana, taarifa kuhusu namna sahihi ya kuzitumia, na upatikanaji wa tiba baada ya kupata maambukizi zinachukuliwa;
(f) hatua madhubuti za kupunguza tabia zenye kuleta hatari kubwa, pamoja na vikundi vya watu walio katika hatari kubwa zaidi, kwa mtazamo wa kupunguza matukio ya VVU zinachukuliwa; na
(g) inapangwa mikakati ya kupunguza madhara kwa kuzingatia mwongozo uliochapishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Kimataifa la Kupambana na VVU/UKIMWI Duniani (UNAIDS) na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Madawa ya Kulevya na Uhalifu (UNODC) na miongozo mingine husika.

*Tiba na huduma*

17. Wanachama (wa Shirika la Kazi Duniani) wahakikishe kuwa sera na programu zao za kitaifa kuhusu afya mahali pa kazi zimeamuliwa kwa kushauriana na waajiri na wafanyakazi na wawakilishi wao na zimeunganishwa na huduma za afya kwa umma. Waingilie kati kwa njia sahihi na zinazofaa kuzuia VVU na UKIMWI na kudhibiti athari zake.

18. Wanachama wahakikishe kuwa wafanyakazi wanaoishi na VVU na wategemezi wao wananufaika kwa kupata huduma kamili za afya, iwe huduma hii inatolewa chini ya mfumo wa huduma ya afya ya umma, hifadhi ya jamii au bima binafsi au mifumo mingine. Wanachama pia wahakikishe inatolewa elimu na kuamsha ufahamu wa wafanyakazi ili kuwawezesha kupata huduma ya afya.

19. Watu wote walioguswa na Pendekezo hili, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wanaoishi na VVU na familia na wategemezi wao, watastahili kupatiwa huduma za afya. Huduma hizi zijumuishe upatikanaji wa bure au kwa gharama nafuu huduma za:
(a) ushauri na kupima kwa hiari;
(b) matibabu kwa kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI na kupata elimu, habari na msaada;
(c) kupata lishe sahihi wakati wote na matibabu;
(d) kutibiwa magonjwa nyemelezi na magonjwa yaambukizwayo kwa ngono, na magonjwa mengine yoyote yanayohusiana na VVU, hususan kifua kikuu; na
(e) programu za msaada na kinga kwa watu wanaoishi na VVU, pamoja na msaada wa kisaikolojia.

20. Kusiwe na ubaguzi dhidi ya wafanyakazi au wategemezi wao kutokana na kuwa au kutambulika kuwa na VVU katika kupata huduma za hifadhi ya jamii na bima kazini, au kuhusiana na mafao chini ya mifuko hiyo, ikiwa ni pamoja na huduma ya afya na walemavu, na mafao ya kifo na mafao kwa ndugu waliobakia.

*Msaada*

21. Programu za huduma na msaada zichukue hatua za kuwapangia kazi wanazomudu mahali pa kazi watu wanaoishi na VVU au magonjwa yanayohusiana na VVU, kwa kuzingatia kwa makini mazingira ya nchi. Kazi ipangwe kwa njia ambayo itaweza kufanywa na watu wenye maambukizi ya VVU na UKIMWI, na vilevile kuzingatia madhara ya matibabu yanayoweza kutokea.

22. Wanachama wahimize kuwabakiza kazini na kuwaajiri watu wanaoishi na VVU. Wanachama wafikirie kutoa msaada kupitia vipindi vya ajira na ukosefu wa ajira, ikiwezekana pamoja na kutoa fursa za kuzalisha kipato kwa watu wanaoishi na VVU au watu walioathirika na VVU au UKIMWI.

23. Pale ambapo uhusiano wa moja kwa moja unaweza kuanzishwa kati ya kazi na hatari ya maambukizi, UKIMWI na maambukizi ya VVU lazima itambuliwe kama ugonjwa unaohusiana na kazi au ajali, kulingana na taratibu na fasili za kitaifa, na kulingana na Orodha ya Pendekezo la Magonjwa ya Kazi, 2002, na vilevile sheria nyingine husika za Shirika la Kazi Duniani.

*Kupima, faragha na siri*

24. Upimaji lazima ufanyike kwa hiari na bila kushurutishwa na programu za upimaji lazima ziheshimu mwongozo wa kimataifa kuhusu kutunza siri, kutoa ushauri na kuridhia.

25. Upimaji wa VVU au njia nyingine za kuchunguza VVU zisiwe lazima kwa wafanyakazi, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wahamiaji, watafuta kazi na wanaoomba kazi.

26. Matokeo ya upimaji wa VVU yatunzwe kwa siri na yasihatarishe upatikanaji wa kazi, kipindi cha ajira, uhakika wa kazi au fursa za kujiendeleza

27. Wafanyakazi, pamoja na wafanyakazi wahamiaji, watafuta kazi na wanaoomba kazi, wasitakiwe na nchi zao, nchi za mpito au wanakoenda kutoa habari zinazowahusu kuhusiana na VVU au za wengine. Upatikanaji wa habari hizi ufuate kanuni za kutunza siri kulingana na kanuni za utendaji za ILO kuhusu utunzaji wa taarifa binafsi za wafanyakazi, za mwaka 1997, na viwango vingine vya kimataifa vya utunzaji wa taarifa.

28. Wafanyakazi wahamiaji, au wale wanaotaka kuhamia kwa ajili ya ajira, wasizuiliwe kuhamia na nchi zao, za mpito au nchi wanakoenda kutokana na hali yao halisi au kwa kutambulika kuwa na VVU.

29. Wanachama wawe na taratibu rahisi za kusuluhisha migogoro ambazo zitahakikisha kuwa matatizo ya wafanyakazi yanatatuliwa iwapo haki zao zilizotajwa hapo juu zimekiukwa.

*Usalama na afya kazini*

30. Mazingira ya kazi lazima yawe ya usalama na afya, ili kuzuia maambukizi ya VVU mahali pa kazi, kwa kuzingatia Mkataba wa Usalama na Afya Kazini, 1981, Mkataba wa Mfumo wa Ukuzaji wa Usalama na Afya Kazini, 2006, na Pendekezo, 2006, na sheria nyingine husika za kimataifa, kama vile nyaraka za pamoja za Shirika la Kazi Duniani (ILO) na Shirika la Afya Duniani (WHO).

31. Hatua za kulinda usalama na afya ili kuzuia wafanyakazi kuwa katika mazingira hatarishi ya VVU kazini zijumuishe kuchukua tahadhari kwa ujumla, hatua za kuzuia ajali na madhara, kama vile hatua zinazochukuliwa na shirika, udhibiti wa kiuhandisi na taratibu za kazi, vifaa vya kujikinga, vinavyotakiwa, hatua za udhibiti wa mazingira na matibabu baada ya kupata ugonjwa na hatua nyingine za usalama ili kupunguza hatari ya kupata VVU na kifua kikuu, hususan katika kazi zenye hatari kubwa zaidi, ikiwa ni pamoja na sekta ya huduma za afya.

32. Kunapokuwa na uwezekano wa kupata maambukizi ya VVU kazini, wafanyakazi wapatiwe elimu na mafunzo kuhusu njia za maambukizi na hatua za kuzuia kupata maambukizi na ugonjwa. Wanachama wachukue hatua za kuhakikisha kuwa huduma za kinga, usalama na afya zinatolewa kulingana na viwango husika.

33. Hatua z a kuamsha ufahamu zisisitize kuwa VVU haviambukizwi kwa kugusana na kuwa kuwepo kwa mtu anayeishi na VVU isichukuliwe kama hatari ya mahali pa kazi.

34. Huduma za afya kazini na taratibu za mahali pa kazi zinazohusu usalama na afya kazini ziangalie VVU na UKIMWI, kwa kuzingatia Mkataba wa Huduma za Afya Kazini, 1985, na Pendekezo la 1985, *Miongozo ya Pamoja ya ILO/WHO kuhusu huduma za afya na VVU/UKIMWI*, 2005, na marudio yoyote yanayofuata, na sheria nyingine zozote za kimataifa.

### *Watoto na vijana*

35. Wanachama wachukue hatua za kupambana na utumikishwaji wa watoto na usafirishaji haramu wa watoto ambao unaweza kuwa umesababishwa na vifo au ugonjwa wa wanafamilia au walezi kutokana na UKIMWI na kupunguza mazingira hatarishi ya VVU kwa watoto, kwa kuzingatia Azimio la ILO kuhusu Kanuni na Haki za Msingi Kazini, 1998, Mkataba wa Umri Mdogo, 1973, na Pendekezo la, 1973, na Mkataba wa Utumikishwaji wa Watoto Kazi za Hatari, 1999, na Pendekezo la, 1999. Hatua maalum zichukuliwe ili kuwalinda watoto hawa kutokana na unyanyasaji wa kijinsia na utumikishwaji katika ngono.

36. Wanachama wachukue hatua za kuwalinda wafanyakazi vijana dhidi ya maambukizi ya VVU, na katika kushughulikia masuala ya VVU na UKIMWI, waingize mahitaji maalum ya watoto na vijana kwenye sera na programu za taifa. Sera na programu hizi zijumuishe elimu ya afya ya ngono na uzazi, hususan usambazaji wa habari kuhusu VVU na UKIMWI kupitia mafunzo ya ufundi na katika programu za ajira na huduma kwa vijana.

## V. UTEKELEZAJI

37. Sera na programu za taifa kuhusu VVU na UKIMWI na ulimwengu wa kazi:

(a) zipewe uzito, kwa kushauriana na vyama vya waajiri na wafanyakazi vyenye uwakilishi mkubwa na pande nyingine husika, ikiwa ni pamoja na vyombo husika vya umma na binafsi vya afya kazini, kwa njia moja au mchanganyiko wa njia zifuatazo:
   - i. sheria na kanuni za kitaifa;
   - ii. makubaliano ya pamoja;
   - iii. sera na programu za utekelezaji za taifa na za mahali pa kazi; na
   - iv. mikakati ya kisekta, kwa kuzingatia zaidi sekta ambapo watu wanaolindwa na Pendekezo hili wapo katika hatari kubwa zaidi;

(b) zijumuishe mamlaka ya mahakama zinazoshughulikia masuala ya kazi, na mamlaka ya usimamizi wa masuala ya kazi katika kupanga na kutekeleza sera na programu, na kwa hali hii mafunzo yatolewe kwao;

(c) sheria na kanuni za kitaifa zitaje hatua za kuchukua kushughulikia uvunjaji wa faragha na siri na ulinzi mwingine unaotolewa chini ya Pendekezo hili;

(d) kuhakikisha kuwepo ushirikiano na mawasiliano miongoni mwa mamlaka ya umma na huduma binafsi husika, pamoja na programu za bima na mafao au programu za aina nyingine;
(e) kukuza na kusaidia biashara zote kutekeleza sera na programu za taifa, ikiwa ni pamoja na kupitia mlolongo wao wa ugawaji na mitandao ya usambazaji, kwa kushirikisha vyama vya waajiri na wafanyakazi na kuhakikisha kuwa mashirika yanayoendesha shughuli zao kwenye kanda za usafirishaji bidhaa nje ya nchi yanafuata masharti hayo;
(f) kuendeleza majadiliano ya kijamii, ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri na kujadiliana, kulingana na Mkataba wa Majadiliano ya Utatu (Viwango vya Shirika la Kazi Duniani), 1976, na njia nyingine za ushirikiano miongoni mwa mamlaka za serikali, waajiri wa sekta ya umma na binafsi na wafanyakazi na wawakilishi wao, kwa kuzingatia mitazamo ya wataalamu wa afya kazini, wataalamu katika VVU na UKIMWI, na pande nyingine pamoja na vyama vinavyowawakilisha watu wanaoishi na VVU, mashirika ya kimataifa, mashirika husika ya kijamii na mfumo wa uratibu nchini;
(g) kuanzishwa, kutekelezwa, kupitiwa upya na kuboreshwa mara kwa mara, kwa kuzingatia maendeleo ya hivi karibuni ya kisayansi na kijamii na haja ya kuingiza masuala ya jinsia na utamaduni kwenye sera na programu;
(h) kuratibiwa, miongoni mwa mambo yote, sera na programu za kazi, hifadhi ya jamii na afya; na
(i) kuhakikisha kuwa Wanachama wanapanga njia zinazofaa kwa ajili ya utekelezaji wake, kwa kuzingatia vya kutosha hali ya kitaifa, na vilevile uwezo wa waajiri na wafanyakazi.

*Majadiliano ya kijamii*

38. Utekelezaji wa sera na programu kuhusu VVU na UKIMWI uzingatie ushirikiano na kuaminiana miongoni mwa waajiri na wafanyakazi na wawakilishi wao, na serikali, kwa kuwashirikisha kikamilifu, mahali pao pa kazi, watu wanaoishi na VVU.

39. Vyama vya waajiri na wafanyakazi viamshe ufahamu wa VVU na UKIMWI, ikiwa ni pamoja na kutoa kinga na kutobagua, kupitia njia ya kutoa elimu na taarifa kwa wanachama wake. Haya yawe masuala muhimu ya kuzingatia kijinsia na kiutamaduni.

*Elimu, mafunzo, habari na ushauri*

40. Mafunzo, maelekezo ya masuala ya usalama na mwongozo wowote muhimu mahali pa kazi unaohusiana na VVU na UKIMWI utolewe kwa njia iliyo wazi kwa wafanyakazi wote, walioajiriwa upya au wafanyakazi wasio na uzoefu, wafanyakazi vijana na watu walio kwenye mafunzo, pamoja na wale walio katika mafunzo kwa vitendo na wanafunzi wa fani za ufundi. Mafunzo, maelekezo na mwongozo uangalie masuala ya jinsia na utamaduni na yarekebishwe kulingana na sifa za nguvukazi, kwa kuzingatia mambo yanayoweza kuleta hatari kwa nguvukazi.

41. Zitolewe habari za kisayansi, kijamii na kiuchumi zinazoenda na wakati na, ikiwezekana, elimu na mafunzo kuhusu VVU na UKIMWI itolewe kwa waajiri, mameneja na wawakilishi wa wafanyakazi, ili iwasaidie katika kuchukua hatua sahihi mahali pa kazi.

42. Wafanyakazi, pamoja na wale walio katika mafunzo kwa vitendo na wanafunzi wa fani za ufundi; pia wale wanaojitolea wapatiwe habari za kuamsha ufahamu na mafunzo sahihi kuhusu taratibu za kudhibiti maambukizi ya VVU katika muktadha wa ajali mahali pa kazi na huduma ya kwanza. Wafanyakazi ambao kazi zao zinawaweka katika hatari ya kugusa damu ya binadamu, bidhaa za damu na viowevu vingine vya mwilini lazima wapate mafunzo ya ziada katika kuzuia maambukizi, taratibu za kutoa taarifa za maambukizi na matibabu baada ya maambukizi.

43. Wafanyakazi na wawakilishi wao wana haki ya kupewa taarifa na kushauriwa kuhusu hatua zilizochukuliwa kutekeleza sera na programu za mahali pa kazi zinazohusiana na VVU na UKIMWI. Wafanyakazi na wawakilishi wa wafanyakazi washiriki katika ukaguzi wa mahali pa kazi kulingana na taratibu za kitaifa.

*Huduma za umma*

44. Nafasi ya huduma za usimamizi wa kazi, pamoja na ukaguzi wa kazi, na uongozi wa mahakama zenye mamlaka katika masuala ya kazi, katika kushughulikia VVU na UKIMWI, zinatakiwa kupitiwa upya na, ikiwezekana, ziimarishwe.

45. Mifumo ya afya ya umma iimarishwe na kufuata *Mwongozo wa Pamoja wa ILO/WHO kuhusu huduma za afya na VVU/UKIMWI*, 2005, na mapitio yoyote yanayofuata, ili kusaidia kuhakikisha kinga, matibabu, huduma na msaada unapatikana kwa wingi na kupunguza mzigo wa ziada wa huduma za umma, hususan kwa wafanyakazi wa sekta ya afya, unaosababishwa na VVU na UKIMWI.

*Ushirikiano wa kimataifa*

46. Wanachama washirikiane, kupitia mikataba ya pande mbili au pande mbalimbali, kupitia ushiriki wao kwenye mfumo wa pande mbalimbali au kupitia njia nyingine zinazofaa, ili kufanya Pendekezo hili liweze kutumika.

47. Hatua za kuhakikisha upatikanaji wa kinga, matibabu, huduma za VVU na msaada kwa wafanyakazi wahamiaji zichukuliwe na nchi walikotoka, wanapopita na kule wanakoenda, na makubaliano yafikiwe miongoni mwa nchi husika, inapowezekana.

48. Ushirikiano wa kimataifa uhimizwe miongoni mwa Wanachama, vyombo vyao vya kitaifa kuhusu VVU na UKIMWI na mashirika husika ya kimataifa na ujumuishe ubadilishanaji wa habari kuhusu hatua zote zilizochukuliwa kupambana na kuenea kwa VVU.

49. Wanachama na mashirika ya pande mbalimbali yazingatie kwa makini uratibu na raslimali muhimu kutosheleza mahitaji ya nchi zote, hususan nchi zilizoenea ugonjwa zaidi, katika kuandaa mikakati na programu za kimataifa kwa ajili ya kutoa huduma za kinga, matibabu, matunzo na msaada unaohusiana na VVU.

50. Wanachama na mashirika ya kimataifa watafute njia ya kupunguza bei ya aina zote za madawa kwa ajili ya kinga, matibabu na huduma kwa ajili ya maambukizi yaliyosababishwa na VVU na magonjwa mengine nyemelezi na saratani zinazohusiana na VVU.

## VI. UFUATILIAJI

51. Wanachama waweke utaratibu sahihi au watumie taratibu zilizopo, kwa ajili ya kufuatilia maendeleo kulingana na sera yao ya taifa ya VVU na UKIMWI na ulimwengu wa kazi, na vilevile kwa ajili ya kutoa ushauri kuhusu upitishaji na utekelezaji wake.

52. Vyama vyenye uwakilishi mkubwa wa waajiri na wafanyakazi viwakilishwe, kwa usawa, katika utaratibu wa kufuatilia maendeleo kulingana na sera ya taifa. Kwa kuongezea, vyama hivi viombwe kutoa ushauri chini ya utaratibu huu mara kwa mara iwezekanavyo, kwa kuzingatia mawazo ya vyama vya watu wanaoishi na VVU, ripoti za wataalamu au tafiti za kitaalamu.

53. Wanachama wakusanye kwa kiwango kinachowezekana taarifa na takwimu kamili na kufanya utafiti kuhusu maendeleo katika ngazi za kitaifa na kisekta kuhusiana na VVU na UKIMWI katika ulimwengu wa kazi, kwa kuzingatia idadi ya wanawake na wanaume na sifa nyingine husika.

54. Pamoja na kutoa ripoti chini ya ibara ya 19 ya Katiba ya Shirika la Kazi Duniani, mapitio ya mara kwa mara ya hatua zilizochukuliwa kwa kuzingatia Pendekezo hili zaweza kuingizwa kwenye ripoti za kitaifa kwenda UNAIDS na ripoti chini ya sheria husika za kimataifa.



ISBN 978-92-2-923819-7